# Upekee wa Nomino Mahususi: Uchunguzi Kifani wa Majina ya Mahali ya Kihaya

*A. Buberwa*

*Ikisiri*

Licha ya wataalamu mbalimbali kama Massamba (2004), Habwe na Karanja (2004)), Matei (20008) na Kihore na wenzie (2009) kudai kwamba nomino mahususi yakiwemo majina ya mahali hurejelea vitu mahususi au maalumu, nomino za mahali za Kihaya[1] zinaibua sura mpya inayohitaji kuzitazama nomino hizo kwa jicho pevu zaidi. Kwa mfano, **Itako** ni jina lenye maana ya 'tako' lakini hurejelea pia kijiji kimoja kinachopatikana katika kata ya Ruhunga, Wilaya ya Bukoba Vijijini. Je, umahususi wa nomino mahususi ni upi? Ili kujibu swali hili makala haya yanaangazia kuwepo kwa majina ya mahali ya Kihaya yanayorejelea vitu tofautitofauti na sababu zinazochochea hali hiyo. Madai yanayoongoza makala haya ni kwamba mstari unaotenganisha nomino mahususi au nomino za pekee na nomino za kawaida ni mwembamba na wakati mwingine ni vigumu kuutambua nje ya muktadha husika. Makala haya yamehusisha data iliyokusanywa katika utafiti uliofanyika katika wilaya ya Bukoba (V), kata za Ruhunga, Rubale, Mikoni, Butelankuzi, na Kikomero. Sehemu ya data hiyo imetumika katika kuandaa tasnifu ya Umahiri ya Buberwa (2010).

## 1.0 Utangulizi

Nomino ni neno linalotaja kitu (mfano kiti, meza, na chungu), kiumbe (mfano mtu, ndege, mnyama au jina la mtu kama Asha), sehemu (mfano Tanzania, Kinondoni na Tabora), tendo (mfano usukani na uainishaji) na hali (mfano, majonzi na furaha) (Massamba, 2004). Kwa msingi wa mgawanyo wa nomino kwa kuzingatia makundi makuu, nomino zote zinaweza kugawika katika makundi matatu ambayo ni *nomino jumuishi* (nomino za kawaida), *nomino mahususi* (nomino za pekee) na *nomino kikundi* (nomino za majina ya jamii) (Kihore na wenzie, 2009). Kwa kuwa lengo la makala haya si kushughulikia aina zote za nomino, tutatoa ufafanuzi wa kina kuhusu nomino mahususi na nomino za kawaida au nomino jumuishi kama sehemu ya utangulizi kuhusu upekee wa nomino mahususi za Kihaya.

## 2.0 Dhana ya Nomino Mahususi na Nomino za Kawaida

Nomino mahususi ni tafsiri ya istilahi ya Kiingereza *proper nouns*. Istilahi hii imefasiliwa na wataalamu mbalimbali wa isimu. Massamba (2004) kwa mfano, amefasili nomino mahususi kuwa ni majina yanayobainisha dhana, vitu au viumbe maalumu. Majina hayo ni pamoja na majina ya watu (mfano Magesa, Yusufu), majina ya mahali (mfano Dar es Salaam, Tanga), majina ya siku (mfano Jumatatu, Jumanne) na majina ya miezi (mfano, Januari, Machi). Fasili

---

[1] Lugha ya Kihaya ni Lugha ya Kibantu inayozungumzwa Kaskazini-Mashariki mwa Tanzania, hususan katika Mkoa wa Kagera.

hii imeungwa mkono na watafiti wengine kama Kihore na wenzie (2009) na Matei (2008). Aidha, wataalamu wengine kama Habwe na Karanja (2003) hutumia istilahi ya *nomino za pekee* kuzirejelea nomino hizo.

Nomino za kawaida kwa upande mwingine, ni tafsiri ya istilahi ya Kiigereza *common nouns*. Massamba (2004) anafasili istilahi hii kuwa ni majina yasiyobainisha wazi vitu vinavyotajwa kama kitabu, kalamu, ugonjwa na kadhalika. Aidha, nomino za kawaida zinafasiliwa kama nomino ambazo hutaja mtu, jambo, kitu au wazo ambalo si maalumu (Matei, 2008). Matei anaongeza kuwa nomino za kawaida hutaja kitu kwa ujumla bila kukitofautisha zaidi na nomino mahususi ambazo hutaja vitu kwa upekee na kuvitofautisha na vitu vingine vya aina yake. Kwa kuwa si lengo la makala haya kujadili kama istilahi ipi ndio sadifu, makala haya yametumia istilahi za *nomino mahususi* na *nomino za kawaida* kwa kuamini kwamba istilahi hizi zitafaa kwa azma tuliyonayo katika kutimiza malengo ya makala.

Kwa kuwa zipo aina nyingi za nomino mahususi, makala haya yameshughulikia nomino mahususi za Kihaya zinazohusisha majina ya mahali tu, hususan ya kata, vijiji na vitongoji katika wilaya ya Bukoba vijijini. Sehemu inayofuata inazingatia dhana ya upekee au umahususi wa majina ya mahali ya Kihaya.

## 3.0 Upekee wa Nomino za Mahali za Kihaya

Licha ya wanaisimu mbalimbali waliotajwa awali (Taz.§ 2.0) kudai kuwa nomino mahususi hutaja vitu maalumu, mahususi au vya kipekee ambavyo hujitofautisha na vitu vingine, nomino za mahali katika Kihaya zinaibua dhana tofauti na madai hayo. Nomino hizi hutaja vitu mbalimbali, sanjari na kutaja mahali au sehemu mahususi. Hali hii husababisha ugumu katika kutambua dhana inayodokezwa na umbo-jina fulani endapo msikilizaji hatazingatia muktadha husika wa mazungumzo. Ufafanuzi zaidi kuhusu hoja hii umeshughulikiwa katika sehemu zinazofuata.

### 3.1 Nomino za Mahali kama Majina ya Watu

Tafiti mbalimbali zilizofanywa na wataalamu mbalimbali kuhusu nomino za mahali zimedhihirisha kuwa baadhi ya majina ya mahali hutokana na majina ya watu. Rye (2006), kwa mfano, amefanya utafiti katika majina ya Kianglikana ya Norfolk na Suffolk. Utafiti huo umedhihirisha kuwa majina ya mahali hutokana na majina ya watu wa kwanza kuishi katika eneo linalohusika. Madai haya hayatofautiani na yale ya Levitt (1959) ambaye amechunguza mfumo wa uteuzi wa majina ya mahali ya Uingereza katika lugha ya Kiingereza na kutaja kuwa baadhi ya majina ya mahali hudokeza kuhusu majina ya watu walioishi katika sehemu hiyo. Kama ilivyoelezwa na watalaamu hawa kuhusu majina ya mahali ya Norfolk, Suffolk na England baadhi ya majina ya mahali ya Kihaya pia

hutokana na majina ya watu walioishi katika eneo hilo. Chunguza mifano ifuatayo:

**Mfano 1:**
i) Rugambwa (jina la mtu)
ii) Mujunangoma (jina la mtu)

Majina haya yakitajwa nje ya muktadha yanaweza kuibua utata kwa msikilizaji. Majina haya hurejelea watu au vijiji ambavyo vinapatikana katika kata ya Ruhunga, katika wilaya ya Bukoba Vijijini. Aidha, ipo shule ya sekondari inayojulikana kwa jina la Rugambwa katika wilaya ya Bukoba Mjini. Lengo hapa si kuonesha uwepo wa jina moja linalorejelea sehemu tofauti bali kuangazia utelezi wa dhana ya upekee au umahususi wa nomino za mahali za Kihaya. Hivyo basi, mifano iliyotajwa katika mfano (1) inadhihirisha kuwa majina ya mahali ya Kihaya siyo bainifu (mahususi) nje ya muktadha kwani ni vigumu kutambua kirejelewa chake. Hata hivyo, suala la jina moja kurejelea sehemu zaidi ya moja linahitaji uchunguzi wa kina ili kubaini sababu zinazochochea hali hiyo.

## 3.2 Nomino za Mahali kama Majina ya Mimea

Baadhi ya nomino za mahali za Kihaya hutokana na majina ya mimea mbalimbali inayopatikana katika kata, kijiji au kitongoji mahususi. Kwa hakika, nomino hizo huwa na maumbo yaleyale ya majina ya mimea husika kiasi kwamba ni vigumu kutambua kama msemaji anakusudia kutaja mahali au mmea, hasa pale muktadha usipobainisha kwa mifano majina ya vijiji na vitongoji. Mifano ifuatayo inashadidia hoja hii:

**Mfano 2:**

| | **Majina ya Mahali** | **Maana Inayodokezwa** |
|---|---|---|
| i) | Kabiriizi (kijiji) | mti mdogo unaojulikana kwa jina la *mubiriizi* |
| ii) | Kagemu (kitongoji) | mgomba mdogo |
| iii) | Ruteete (kijiji) | aina ya nyasi |
| iv) | Misheeshe (kijiji) | miti mingi inayojulikana kama *misheeshe* |

Nomino hizi za mahali zitaainishwa kuwa majina ya mahali pale tu yatakapokuwa katika maandishi kwa kuwa yataandikwa kwa kuanza na herufi kubwa. Kwa kutaja tu majina hayo yakiwa pwekepweke ni vigumu kujua kinachorejelewa. Katika utafiti uliofanywa na Schotsman (2003) imeelezwa kuwa baadhi ya majina ya vituo vya daladala katika jiji la Dar es salaam yametokana na majina ya mimea ama miti mbalimbali. Kutokana na maelezo

haya, upekee wa nomino za mahali za Kihaya na hata lugha nyingine kama Kiswahili una uvulivuli.

### 3.3 Nomino za Mahali kama Majina ya Vitu

Baadhi ya nomino za mahali za Kihaya hurejelea vitu mbalimbali kama vile mazao au vyakula, mchanga, mawe na vitu vingine vingi vinavyopatikana katika sehemu inayohusika. Mifano ifuatayo inadhihirisha hoja hii:

**Mfano 3:**

| | **Majina ya Mahali** | **Maana Inayodokezwa** |
|---|---|---|
| i) | Kabaale (kijiji) | jiwe dogo |
| ii) | Rubaale (kata) | mawe madogo madogo |
| iii) | Katoke (kijiji) | ndizi ndogo/nzuri |
| iv) | Kashenye (kijiji) | mchanga mzuri |
| v) | Kahyoro (kijiji) | tupa ndogo/nzuri – kifaa cha kunolea |

Mifano hii inaonesha wazi kuwa nomino za mahali za Kihaya hutokana na nomino za kawaida zinazotaja vitu mbalimbali kama vile mawe, mchanga na tupa. Buberwa (2011) anadokeza kuwa msingi wa nomino za mahali za Kihaya ni nomino za kawaida. Kwa kuwa majina hayo hutokana na nomino za kawaida ni vigumu kutofautisha nomino zipi ni za kawaida na zipi ni mahususi. Kwa misingi hiyo, mstari unaotenganisha nomino mahususi na nomino za kawaida ni mwembamba kiasi kwamba ni vigumu kuweka mpaka kati ya aina hizo za nomino bila kuhusisha na muktadha wa kimazungumzo au wa kimaandishi.

### 3.4 Nomino za Mahali kama Majina ya Viungo vya Mwili

Baadhi ya nomino ya mahali za Kihaya hurejelea sehemu za mwili wa binadamu kama kisogo, kichwa, tako na macho. Tazama mifano ifuatayo:

**Mfano 4:**

| | **Majina ya Mahali** | **Maana Inayodokezwa** |
|---|---|---|
| i) | Omunkombo (kijiji) | kwenye kisogo |
| ii) | Kitwe (kata) | kichwa-kikubwa/kibaya |
| iii) | Itako (kijiji) | tako |
| iv) | Kaisho (kitongoji) | jicho-dogo |

Hali hii inaelezwa pia na Ash (*hakijachapishwa*) kuwa baadhi ya nomino za mahali za lugha za *Yuwaalaraay, Yuwaaliyaay* na *Gamilaraay*[2] hutokana na majina ya viungo vya binadamu. Ash anafafanua dai hili kwa kutoa mifano kama *Yangledool* lenye maana ya 'kuma ndogo', *Terewah* lenye maana ya 'mguu mwembamba' na *Nullawa* lenye maana ya 'uso mwembamba/sura

[2] Yuwaalaraay, Gamilaraay na Yuwaaliyaay ni lugha zinazopatikana kaskazini-magharibi mwa jimbo jipya la Wales kusini nchini Australia.

ndogo'. Madai haya yanadhihirisha kuwa umahususi wa nomino za mahali unaleta uvulivuli kwani nomino hizo hurejelea pia sehemu fulani na vitu vingine tofautitofauti kiasi kwamba ni vigumu kutofautisha kirejelewa husika nje ya muktadha maalumu.

**4.0 Sababu Zinazochochea Uvulivuli kuhusu Upekee wa Nomino za Mahali**
Wataalamu mbalimbali kama vile Cameron (1961), Powicke (1954), Roden (1974), Msanjila na wenzie (2009), Rayburn (2010), Buberwa (2010) na wengineo wamechunguza nomino za mahali kwa kutumia mkabala wa kiisimujamii na kubaini kuwa kuna sababu za kiisimujamii zinazosababisha uteuzi wa majina fulani yanayorejelea sehemu fulanifulani. Sababu zinazobainishwa ni pamoja na kuwepo kwa aina fulani ya mimea, wanyama, mazao, watu wa koo au taifa fulani, milima, miamba na matukio muhimu yaliyotokea katika jamiilugha hiyo.

Kwa hakika nomino za mahali katika Kihaya hazitokei kwenye ombwe. Hutokana na majina mbalimbali yanayotaja vitu kama mawe, miti, mimea, mchanga, mazao, vyakula, watu ama vitu vingine vingi kama mifano iliyowasilishwa katika makala haya inavyoonesha. Ijulikane kwamba siyo kila kitu kinachopatikana katika kata, kijiji au kitongoji hutumika katika kuunda majina ya sehemu hizo. Uteuzi wa majina hayo huzingatia sifa fulani za vitu au watu ambao majina yao huteuliwa kuwa majina ya sehemu inayohusika. Majina hayo hujumuisha majina ya watu maarufu, wingi wa mimea au miti, uzuri au ubaya wa vitu mbalimbali na matukio yaliyoonekana kuwa ya kustaajabisha. Licha ya kuteuliwa kuwa majina ya kata, vijiji au vitongoji, majina hayohayo huendelea kurejelea vitu vingine kama ilivyobainishwa awali. Hali hii kusababisha dhana ya upekee wa nomino za mahali za Kihaya kupotea.

Ni dhahiri kuwa nomino za Kihaya zinazorejelea sehemu, hurejelea pia vitu vingine kama mifano mbalimbali katika makala haya inavyothibitisha. Hivyo basi, madai kuwa nomino mahususi, yakiwemo majina ya mahali hutaja vitu maalumu au mahususi na kuvitofautisha vitu hivyo na vitu vingine vya aina yake ni telezi kwa upande wa majina ya mahali ya Kihaya. Hii ni kwa sababu majina ya mahali ya Kihaya ambayo yangetajwa kuwa mahususi, hutokana na majina ya kawaida na hivyo, kusababisha majina hayo kutokutofautiana na nomino za kawaida pale yanapotamkwa nje ya muktadha maalumu au mahususi. Kuyatazama majina ya mahali ya Kihaya kama nomino mahususi pwekepweke kwa kuzingatia kirejelewa ni suala tata na gumu kuelezeka kwani majina hayo hurejelea sehemu na vitu vingine ambavyo kwavyo majina hayo ya mahali huundwa.

## 5.0 Hitimisho

Makala haya yameeleza kwa ufupi utelezi wa dhana ya upekee wa nomino mahususi hususan zile zinazotaja mahali au sehemu. Imethibitika kwamba majina ya mahali katika Kihaya hutaja sehemu na vitu vingine tofauti, ambavyo kwavyo, majina hayo yameundwa. Wakati huohuo, imedhihirika kwamba jina moja la mahali huweza kurejelea sehemu tofautitofauti (Taz. § 3.1). Imehitimishwa kwamba mstari unaotenganisha nomino mahususi hasa zinazorejelea mahali husika na nomino za kawaida ni mwembamba sana kiasi kwamba ni vigumu kutofautisha aina hizo za nomino. Hata hivyo, tafiti zaidi zinahitajika ili kuchunguza kwa kina uainishaji wa nomino katika lugha ya Kihaya na katika lugha nyingine za Kibantu na zisizo za Kibantu badala ya kuzitazama nomino mahususi kama vipengele pwekepweke ambavyo ni maalumu na vya kipekee. Upekee huo unadhamiwa una uvulivuli na hivyo, unahitaji muktadha maalumu ili kuweza kuzibainisha.

## Marejeo


Ash, A. (hakijachapwa). *Place names in Yuwaalaray, Yuwaaliyaay and Gamilaraay Languages of North-West New South Wales*.

Buberwa, A. (2011). "Viambishi-ngeli katika Nomino za Pekee: Mifano Kutoka katika Majina ya Mahali ya Kihaya." *Kiswahili,* Juz. 74 Dar es Salaam: TUKI

Buberwa, A. (2010). Investigating Sociolinguistic Aspects of Place Names in Ruhaya in North-Western Tanzania. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Cameron, K. (1961). *English Place Names*. London: Batsford.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix.

Katz, J.J (1985). *Philosophy of Language*: London: Oxford University Press

Kihore, Y. M na wenzie, (2008). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu* (SAMIKISA). Dar es Salaam: TUKI.

Levitt, J. (1959). *The Spell of Words.* London: Darwen Finlayson.

Lyons, J. (1984). *Language and Linguistics: An Introduction.* Cambridge: Cambridge University Press

Matei, A. K. (2008. *Darubini ya Sarufi: Ufafanuzi Kamili wa Sarufi*. Nairobi: Phoenix Publishers

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Msanjila. Y. P. na wenzie (2009). *Isimujamii: Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: TUKI.

Powicke, F. (1954). Reviewing Armstrong, Mawer, Stenton and Dickins: *The Place Names of Cumberland 1950-1953 in the English Historical Review*, Juz.69, uk..312.

Rayburn, A. (2010). *Place Names* –The Canadian Encyclopedia-Historical-Dominion.

Roden, D. (1974). Some Geographical Implications from the Study of Ugandan Place-names, katika: *East African Geographical Review* no.12 July.uk. 77-86.

Rye, J. (2006). *A Popular Guide to Norfolk Place-names*. Guist Bottom: Larks Press.